TANGAZO LA SERIKALI NA. 105 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MAYA MAYA 'A' YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Maya Maya 'A' ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpangokina wa eneo

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MY1 yenye majira - nukta 809923.166MS, 9357622.967KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa kukatisha barabara ya Maya Maya - Babayu katika uelekeo wa KZ75$^{0}$42''MS kwa umbali wa kilomita 0.92 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MY2 yenye majira - nukta 810819.551MS, 9357853.637KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa MS139$^{0}$19' kwa umbali wa kilomita 0.92 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MY3 yenye majira - nukta 811439.677MS, 9357131.257KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS95$^{0}$ 57''MS kwa umbali wa kilomita 2.19 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MY4 yenye majira - nukta 809870.758MS, 9355590.844KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS116$^{0}$59''MG kwa kukatisha barabara ya Maya Maya – Dodoma kwa umbali wa kilomita 0.76 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MY5 yenye majira - nukta 810819.551MS, 9355843.844KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KS146$^{0}$47''MG kwa umbali wa kilomita 0.55 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MY6 yenye majira - nukta 808772.486MS, 9356276.918KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ116$^{0}$27''MG kwa umbali wa Kilomita 0.86 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MY7 yenye majira - nukta 809148.088MS, 9357053.104KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ146$^{0}$47''MG kwa umbali wa kilomita 0.96 hadi ulipoanzia."

Dodoma
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*